

Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo
kwa Kaziya Kimisheni Ulimwenguni Kote

TOLEO LA MAADHIMISHO YA MIAKA KUMI

UKWELI USIOBADILIKA

Gazeti la Ukweli wa Injili limechapishwa na kusambazwa kwa miaka kumi sasa. Toleo la kwanza lilichapishwa hapo mwaka wa Julai 2012. Katika mwongo uliopita kumekuwa na matukio makubwa na mabadiliko mengi katika jamii. Kumekuwa na matufani mengi, misukosuko ya ardhi, na tsunami ambazo zimepiga nchi nyingi ulimwenguni na kuleta hasara ya mabilioni ya dola (za Marekani) na hata kusababisha vifo vya watu wengi. Ukame nao umedhuru sehemu tofauti tofauti ulimwenguni na watu wengi wanakufa kwa njaa. Nao ugonjwa wa covid19 ulibadilisha maisha ya watu kabisa (kabisa), na kusababisha vifo vya watu zaidi ya milioni sita ulimwenguni.



Maadili ya watu nayo yamezidi kuzorota. Kwa kiwango fulani jambo hili linadhihirika kupitia kwa kukubalika na kupigiwa debe kwa tabia za kishoga kwenye vyombo vya habari, mashule, na katika jamii kwa jumla. Basi mabadiliko yaliyofanyika ulimwenguni ni mengi sana, na siku za usoni zinaonekana kujaa giza totoro. Mfumuko wa bei nao unazidi kupanda juu, na viwango vya riba pia kupanda, na hata bei ya mafuta inazidi kuongezeka mno.

Lakini habari njema za kumsifu Mungu ni kwamba Mungu na Neno lake ni mambo ambayo kamwe hayabadiliki. “Kwa kuwa mimi, BWANA, sina kigeugeu” (Malaki 3:6). Haijalishi mambo yaliyotuzunguka yatageuka kwa kiwango kipi, Mungu kamwe habadiliki. Ni baraka kubwa kwa gazeti hili la Ukweli wa Injili kufikisha miaka kumi ya kupigishwa chapa. Neno la Mungu ambalo gazeti la Ukweli wa Injili linachapisha na

kushiriki kwa watu kamwe halijabadilika katika miaka kumi iliyopita. “Majani yakauka, ua lanyauka; bali neno la Mungu wetu litasimama milele” (Isaya 40:8).

Serikali zimebadilika, huduma (za makanisa) zimeanza na kufikia kikomo, falsafa na itikadi za kibinadamu zimeibuka na kutokomea, lakini ukweli wazidi kudumu. Yesu alisema, “Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima” (Yohana 14:6). Yeye angali njia ya pekee ya kwenda Mbinguni na njia hiyo ni timamu. Siku za usoni za mtoto wa Mungu zitazidi kuwa na baraka, na kila nafsi ambayo ina shauku la kumuishia Mungu imebarikiwa. Damu ya Yesu nayo haijapoteza uwezo

wake, na ukweli huo ungali unaleta uhuru kwa watu ambao wamefungwa dhambini.

Tunamshukuru Mungu kwa ukweli kwamba kungali kuna neema ya mtu kuishi maisha matakatifu, na nguvu za neema zinazidi nguvu za dhambi. Basi ingawa kuna migogoro na misukosuko mingi ulimwenguni, hebu tukumbuke maneno ya Bwana yanayosema kwamba: “Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu” (Yohana 16:33). “Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga” (Yohana 14:27).

Ingawa ulimwengu una misukumo na mabadiliko makubwa lengo la gazeti la Ukweli wa Injili halijabadilika— lengo hilo likiwa kuchapisha Neno la Mungu ambalo kamwe halibadiliki.



“Neno la Mungu ambalo gazeti la Ukweli wa Injili linachapisha na kushiriki kwa watu kamwe halijabadilika katika miaka kumi iliyopita.”

Tembelea Tovuti Yetu

Tahariri
3
Mfuatano wa
Masomo ya Matoleo

2

4

Wafanyi Kazi wa
Ukweli wa Injili
5
Sanaa ya Picha

6

Ripoti ya Jinsi Maisha
ya Watu Yalivyoguzwa

7

Je, Wajua?

Neno Linalofaa kwa
Msimu Huu

8

MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUUSU...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,
Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,
Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,
Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,
I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,
Mt. 25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

Tembelea Tovuti Yetu

www.thegospeltruth.org



Tovuti ya Ukweli wa Injili imehifadhi matoleo yote ya Ukweli wa Injili kwa lugha sita: Kizungu, Kihispania, Kijerumani, Kiswahili, Kichichewa, Kitamil, na Kimalayalam.

Matoleo ya hapo mbeleni yana mafundisho ya kidini yanayohusiana na masomo tofauti tofauti. Matoleo hayo yametumika kama mwongozo kwa Wakristo binafsi na hata kwa makundi ya kikanisa kwa ajili ya kujifunza Biblia. Pia yametumika kama ratiba ya masomo ya Biblia kwa wanafunzi wa shule za upili, na kama marejeleo ya watu kujifunza itikadi za Biblia.

Unapofungua toleo la Ukweli wa Injili katika mfumo wa faili ya PDF unaweza kutafuta jambo lolote humo ndani kwa kubonyeza ctrl+F kwenye kompyuta yako. Kila somo kwenye toleo hizo zimwekwa kibinafsi hivi kwamba unaweza kutafuta chochote kilichoandikwa humo.


Hebu jiandikishe kwenye tovuti yetu ili ujulishwe wakati tolea linalofuata la Ukweli wa Injili litakapochapishwa, na ili tutume toleo hilo kwenye anwani yako!

Pata programu ya Ukweli wa Injili

kutoka kwa tovuti ya Google Play Store

Programu ya Ukweli wa Injili inaweza tumiwa na watu ambao wanatumia simu za Android. Unaweza kupata matoleo tofauti tofauti kwa njia ya kuyatafuta kulingana na masomo yaliyomo au maneno makuu yaliyotumika humo.

Kwa sasa tunaunda programu ya lugha ya Kihispania ili tuweze kuizindua.



Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org na ujiandikishe ili uwe ukiumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@thegospeltruth.org

Tahariri



Neno la Bwana likaenea katika nchi ile yote. —Mitume 13:49

Ombi letu na shauku letu lilikuwa (na lingali) kwamba injili ile rahisi ya Bwana wetu Yesu Kristo iweze kuenea katika sehemu zote ulimwenguni. Dini na mashirika ya kibinadamu haziwezi kutosheleza shauku zilizomo katika nafsi za wanadamu. Kuna hitaji kubwa la watu kuweza kusikia na kusoma mafundisho na itikadi safi sisizo na dosari za Neno lake Mungu.

Tunamshukuru Bwana kwamba sasa tunaweza kufurahia miaka kumi ya kuchapisha gazeti hili la Ukweli wa Injili. Kwa kweli jambo hili halijakuwa rahisi au kukosa changamoto zake. Lakini kazi ya Mungu haimpatii mtu nafasi ya kuepuka changamoto, bali inampa mtu nafasi ya kuitikia wito wa Mungu na kufanya mapenzi yake bila kuhesabu gharama ambayo itambidi kulipa. Nakumbuka miaka ishirini na mitano iliyopita nikizungumza kuhusu haja ya kuwepo na gazeti ambalo linaandikwa kwa kukubaliana na itikadi zinazofaa za Kikristo, ili liweze kusambazwa kwa wahudumu ambao walikuwa wakihudumu kwenye misheni zetu. Na miaka mingi baadaye Bwana alitupatia sisi wenyewe jukumu hilo la kuanzisha huduma ya gazeti hili.

Hapa chini kuna nukuu kutoka kwa tahariri ya toleo la kwanza la Ukweli wa Injili hapo mwezi Julai 2012:

Katika huduma ya miaka mingi ambaye nimeifanya kote ulimwenguni nimetambua kuna haja kubwa ya kusaidia uanzishaji wa huduma za kimsingi katika ukweli wa neno. Kusudi letu sio kupata wafuasi au kumfanya mtu fulani 'kujiunga' na kikundi fulani. Lengo letu ni kufunza na kuwahimiza watu kujiunga na Kanisa lolote ambalo linapatikana katika mahali walipo. Kwa njia hiyo umoja unapatikana, wakati watu wanafuata ukweli huku wakiongozwa na Roho . . . Ni kusudi langu na la mke wangu kwamba tuweze kushiriki (nanyi) kupitia kwa neno linaloandikwa kwenye gazeti hili baadhi ya kweli za biblia ambazo ni za kimsingi na ambazo zinaweza kuwasaidia watu wanaomtafuta Mungu kwa kweli, ili waweze kugemezwa katika ukweli huo.

Kwa miaka kumi sasa gazeti la Ukweli wa Injili limechapishwa katika kila robo ya mwaka. Mungu naye amekuwa mwaminifu kupatia huduma hii wasaidizi wa ajabu na pia wasaidizi waliojitolea. Ni kupitia juhudi za watu kama hao hapa Marekani na hata katika nchi za mbali ndiposa huduma hii imeweza kukua na kuwafikia watu wengi zaidi. Tunashukuru watu wote ambao wameunga mkono uchapishwaji wa gazeti la Ukweli wa Injili kwa njia ya maombi na kifedha.

Tunapoinjia kwenye mwongo mwingine wa kuchapisha gazeti hili tuna shauku kubwa ya kuombewa na wewe ili kwamba tupate uvuvio zaidi na kupakwa mafuta na Bwana. Ombi letu ni kwamba katika kila jambo Kristo apate kutukuzwa na Ufalme wake uwe ndio lengo la kila juhudi zetu. Tunaomba kwamba Mungu atafungua milango zaidi na kuwezesha ukweli ushirikishwe kwa nafsi zaidi ambazo zina shauku ya kuatafuta ukweli huo.

Kwa moyo ulio na shukrani, ni mimi,

Michael W. Smith,

Julai 2022

MSHIRIKA MWENZA WA SAFARI YAKO

Katika miaka mitano iliyopita gazeti la Ukweli wa injili limekuwa kitu chenye manufaa makubwa katika kusambaza Injili kati ya watu wanaozungumza lugha ya Kitamil kote katika nchi ya Bara Hindi na sehemu zote za Asia-Pacific. Gazeti hili limetupatia njia ya kufikia idadi kubwa mno ya watu, zaidi ya wale tungeweza kuwafikia kwa kufanya safari za kimisheni. Kwa kweli mbinu hii ya Ukweli wa Injili imekuwa kama mjumbe wa Injili ambaye anatumika mwaka mzima na ambaye haleti vurugu katika sehemu hii ambayo ina upingamizi mkubwa kwa mambo ya Kikristo. Ndiposa kukaanzishwa kazi ya kuchapisha gazeti hili kwa lugha ya Kitamil, kuanzia kwa nakala 500, ikakua na kufikia nakala 1,000, elfu mbili, na kwa sasa tunachapisha nakala 3,500. Hili lilifanyika wakati ambapo sisi tulianza kupata barua na kupigiwa simu na watu wale ambao walikuwa wamepata nakala ya gazeti hili, au kusikia habari ya gazeti hili. Kutoka wakati huo nakala 75,000 za

gazeti hili kwa lugha ya Kitamil zishaweza kusambazwa. Mimi mwenyewe nimeshuhudia matunda ya Injili ambayo yameweza kupandwa kupitia magazeti haya katika sehemu za kimisheni na nimefurahi kushuhudia kwamba Bwana anaweza kufanya kazi na mbegu hizi mwaka mzima, sisi tuwepo au tusikuwepo. Nazo nakala ambazo zimehifadhiwa kwa njia za kidijitali zimekuwa usaidizi mkubwa kwa kuwafundisha Wakristo itikadi za Biblia kuhusiana na masomo mbali mbali, ambayo mimi nimebidiika kufundisha nikiwa katika sehemu zangu za kimisheni. Ndiposa ninakuhimiza wewe kwamba uweze kujiandikisha kwa masomo yako ya kibinafsi ya itikadi za Biblia ili "Mwe tayari siku zote kumjibu . . . habari za tumaini lililo ndani yenu" (1 Petro 3:15). Nami ninaamini kwamba gazeti la Ukweli wa Injili litakuwa mshirika wako mwenza na mwenye manufaa makubwa katika safari yako.

—Ndugu Clint Doolittle

www.thegospeltruth.org



Tutembelee

www.thegospeltruth.org

ili kujiandikisha na

kupata jarida

za mbele.

HIFADHI ZA NAKALA ZA UKWELI WA INJILI

Tolea zote za Ukweli wa injili zinaweza kupatikana kutoka
kwa hifadhi ya tovuti ya www.thegospeltruth.org

Toleo zifuatazo zinaweza kupatikana kwa lugha saba sasa.



1. Injili, Ukweli, Mtu Kuwa Mkweli
2. Wokovu, Dhambi
3. Uhusiano Unaoongozwa na Upendo
4. Ufalme wa Mungu
5. Yesu Kuja Mara ya Pili, Mwisho wa Nyakati
6. Kanisa la Mungu
7. Uwezo wa Adhari za Televisheni na Intaneti
8. Kujazwa na Roho Mtakatifu
9. Glossolalia—Kunena kwa Lugha Nyingine
10. Ubatizo wa Maji
11. Kanuni Kuhusu Wakristo Kuoshana Miguu
12. Mateso ya Kristo; Meza ya Bwana
13. Utakatifu wa Kibinafsi
14. Kupeana Talaka na (Mtu) Kuoia Tena
15. Matendo ya Kusaidia Walio na Shida
16. Jinsi Mtu wa Nje Anavyoonekana
17. Huduma
18. Agano Mbili
19. Mafundisho ya Biblia Kuhusu Fungu la Kumi na Kutoa (Kupeana)
20. Sabato na Siku ya Bwana
21. Muziki Katika Ibada
22. Utatu wa Mungu
23. Kujichunguza Kibinafsi Kuhusu Mambo ya Kiroho
24. Uponyaji wa Kiungu
25. Kufunga
26. Mafundisho ya Biblia Kuhusu Kutompinga Mtu Mwovu – Kutumika Jeshini
27. Usimamizi Bora wa Fedha
28. Usalama wa Milele
29. Kifo cha Kwanza na cha pili – na Ufufuo
30. Sifa
31. Maombi
32. COVID-19 (Toleo Maalum)
33. Kuweka Wachungaji Wakfu
34. Ofisi ya Shemasi
35. Sio wa Ulimwengu (Huu)
36. Wakati wa Shida
37. Nguvu za Mfano
38. Toba Ambayo Inafundishwa Katika Biblia
39. Kuwa Mtu Mkweli
40. Vile Unaweza kujua Mapenzi ya Mungu



Kizungu



Kihispania



Kijerumani



Kitamil



Kichichewa



Kiswahili



Kimalayalam

Walioko Nyuma ya Jukwaa



Timu ya Uchapishaji wa Gazeti la Ukweli wa Injili

Tunatoa shukrani maalum kwa kujitolea na huduma ya miaka mingi ya timu inayochapisha Ukweli wa Injili. Ni jambo linalofurahisha mtu kusoma ujumbe wa Injili kwa lugha ya mama! Hifadhi zinazopatikana kwenye tovuti yetu zinawakilisha kazi kubwa ya miaka mingi ya wafanyi kazi wetu waliojitolea. Baada ya toleo la Kiingereza kuchapishwa watafsiri wetu na wapiga chapa huanza kazi ya kuandaa toleo hilo jipya ili lisambazwe kote ulimwenguni. Maduka ya kupiga chapa yanayopatikana sehemu sehemu yameanzishwa katika nchi tofauti tofauti, na maelfu ya nakala kuchapishwa na kusambazwa katika mikutano na kwenye misheni za uinjilisti kote ulimwenguni. Wakati mwingi sisi hupokea maombi ya kutafsiri kwa lugha zingine mpya lakini tunazuiwa na wakati, fedha, na wafanyi kazi wa kuweza kutimiza lengo hilo. Juu ya yote tunamshukuru Mungu kwa ajili ya wafanyi kazi wetu waaminifu!



Michael Smith

Mhariri Mkuu



René Smith

Mhariri wa Kupanga Miswada/Kiongozi wa Kutafsiri (Marekani)



Aubrey Sorrell

Mpagaji wa Miswada (USA)



Julie Elwell

Msomaji wa profu (Marekani)



Janet McMurrin

Msomaji wa profu (Marekani)



Lenée Sorrell

Mwanatovuti (Marekani)



Irma Sallee

Msomaji wa profu (Marekani)



Damon Sallee

Muundaji wa Programu (USA)



Vanessa Smith

Mtumaji Barua (Marekani)



Tricia Bell

Mtafsiri wa Kihispania (Marekani)



Adrian Glezs

Msomaji wa profu za Kihispania (Mexico)



Ariel Perez

Msomaji wa profu za Kihispania (Mexico)



Ludwig Laukert

Mtafsiri wa Kijerumani (Ujerumani)



Barth Nwachukwu

Mpiga Chapa (Nigeria)



W. S. Vedha

Mhariri wa Kitamil/ Msomaji wa profu (Bara Hindi)



V. J. Gnanarajan

Mchapishaji wa Kitamil/Mtafsiri (Bara Hindi)



V. Selvam

Idara ya Utumaji Barua kwa Lugha ya Kitamil (Bara Hindi)



V. J. Sam Kirubaharan

Mwenye Kutuma Mizigo wa Lugha ya Kitamil (Bara Hindi)



Stephen Mwangi

Mtafsiri wa Kiswahili (Chama cha Biblia cha Kenya)



Alice Ahuga

Mpiga Chapa wa Nakala za Kiswahili (Kenya)



Falistani Kansilanga

Mtafsiri na Mpiga Chapa wa Kichichewa (Chama cha Biblia cha Malawi)



Matthew Joseph

Mhariri wa Kimalayalam/Msomaji profu (Bara Hindi)



Baby Matthew

Mhariri Msaidizi/ Mtafsiri wa Kimalayalam (Bara Hindi)







Biju J. Varghese

Mchapishaji wa Kimalayalam/ Mpangaji wa Kazi (Bara Hindi)

Miaka Kumi ya Uaminifu Wake Mungu

Tulianza kupiga chapa kwa kutumia mashine ndogo ya kupiga chapa ambayo ilikuwa ikifanya kazi pole pole sana, na ambayo tuliweka juu ya meza yetu ya mankuli. Angalau ilituchukua masaa kumi na mawili kupiga chapa hiyo, na ilibidi tuwe makini sana wakati mashine hiyo ikifanya kazi.



"NAAM, TWAKUTAKIA FURAHA YA SIKU YA KUZALIWA EWE UKWELI WA INJILI!"



"Twakutakia furaha ya siku ya kuzaliwa ewe Ukweli wa injili! Tumeweza kuwafikia watu wengi kwa njia yako, hata wale ambao wanaishi mbali sana na miji, ambao hawakuwa na uwezo wa kupata intaneti. Gazeti hili la Ukweli wa Injili ambalo huwa na aya za Biblia ambazo zimeelezewa kwa njia bora limetusaidia sana kufikia kati ya watu 5,000 na 7,000."

"Tumeona watu wengi wakirudi kwetu kupata ukweli zaidi kuhusu viwango vya maisha ambavyo vinatajikana maishani mwa washiriki wa Kanisa la Mungu. Hebu basi tuongane mikono tuombe kwamba gazeti la Ukweli wa Injili lizidi kusambaa zaidi nje ya mipaka yetu, na hata kufika bara zingine. Basi udumu milele ewe Ukweli wa Injili"

Peter Akweyona, Kenya

"Ni jambo linalofaa sisi kumshukuru Mungu kwa ajili ya vile Yeye amedumisha gazeti la Ukweli wa Injili kwa miaka kumi sasa. Tangu mwanzo wake gazeti hili ambalo tunalipenda sana, limetumika katika masomo, na pia kwenye kazi ya uinjilisti. Hapa kwetu kazi ya uinjilisti huwa haijakamilika ikiwa hatuna nakala ya Ukweli wa Injili ya kuwasambazia watu wetu. Lakini, zaidi ya yote, ni kwamba sisi tunashukuru kwa kupata neema ya kuendelea kuchapisha gazeti hili."

Chinwendu Nwachukwu, Nigeria

"Namshukuru Mungu kwa mpango wake wa kuwezesha uchapishaji wa gazeti hili la Ukweli wa Injili. Baada ya kusoma Biblia sisi hutumia wakati kusoma na kufuata maneno ya Mungu kwa njia ya kusoma gazeti hili, na gazeti la Ukweli wa Injili limetusaidia na kutuwezesha kufikia watu katika sehemu mbali mbali bila kuzingatia kama wao wana nakala ya Biblia au la."

"Gazeti la Ukweli wa Injili linatusaidia kubadilisha moyo ya watu wa aina tofauti tofauti, hata wale ambao sio washirika wa kanisa la Mungu. Hapa katika nchi ya Malawi na Mozambique tunamuomba Mungu ili awezeshe kwamba gazeti hili liendeleo kuchapishwa. Kwa kweli tunawatakiya baraka zake Mungu."

Master Gustor, Malawi

"Tumefika hapa kwa maadhimisho ya miaka 10 kwa haraka sana. Tulianza na nakala 500 halafu baadaye, kwa msaada wa Wakristo, tuliweza kuongeza nakala hizi hadi kufikia 3,500. Hii ilitokana na neema yake Mungu."

"Wachungaji hasa wanatumia ujumbe wa Ukweli wa Injili kuhubiri katika ibada zao za Jumapili. Angalau mchungaji ndiye huwa anasoma ujumbe huo, baadaye anasambaza kote kanisani mwake ili uweze kuwafikia waumini wote kupitia kwa mchungaji huyo. Hasa sisi hulisambaza gazeti la Ukweli wa Injili kupitia wachungaji wa hapa kwetu Bara Hindi."

"Kwa kweli sisi hatuasambazi tu magazeti haya kati ya watu wanaozungumza lugha ya Kitamil pekee yake hapa kwenye Bara Hindi, bali pia tunatuma nakala hizo kote ulimwenguni, mahali kote ambako watu wanaozungumza Kitamil wanaishi. Ili kazi hii iweze kuendelea hebu tuombe kwamba tutaweza kuongeza nakala tunazochapisha ili tupate kuisambaza Injili zaidi na zaidi, hadi kuwafikia watu wengi zaidi ulimwenguni kote."

W.S. Vedha (Mhariri wa Lugha ya Kitamil) Bara Hindi

"Kwa kweli sina maneno ze kueleza shukrani zangu kwa Mungu kwa ajili ya gazeti hili la Ukweli wa Injili. Tangu kuanza kuchapishwa gazeti hili, mimi niliona kwamba kuchapishwa kwake kulikuwa njia ya kuweka nguvu ukweli kamili ambao ulipewa watakatifu tangu hapo mwanzo. Kwa mfano: kwa kutumia dakika chache tu mtu anaweza kuelewa vizuri ukweli wote ambao uko kwenye toleo moja la gazeti hili."

"Kwetu sisi hii ni njia rahisi na inayofaa ya kumwongoza mtu kujua kile ambacho Biblia inafundisha. Na zaidi ya hayo baada ya gazeti hili kuchapishwa tunalisambaza katika makusanyiko ya kanisa la Mungu na kuhakikisha kwamba kila mshirika ana nakala yake, na hasa tunalitumia katika kazi ya uinjilisti. Kwa kweli sisi huwapatia gazeti hili wale ambao tunakutana nao kwenye juhudi zetu za uinjilisti wa nyumba kwa nyumba na hata wa barabarani, kama njia ya kusambaza Injili mahali kote. Kusema kweli gazeti hili ndilo tulilolitia wiki jana katika kazi yetu ya uninjilisti ambayo tuliifanya huko Tombia, kwenye Jimbo la Rivers."

"Sisi pia tunalitumia gazeti hili mara nyingi katika Shule Zetu za Jumapili, katika mikutano ya kujifunza Biblia, kwenye sherehe za Mazishi, Ndoa n.k. Na kama nilivyodokeza hapo mbeleni, sasa nimeanza kutuma nakala kadhaa tofauti tofauti za Ukweli wa Injili ambazo zimefungwa pamoja kwa wachungaji watano wa kanisa hili; na nitaendelea kufanya hivyo kulingana na jinsi Bwana atakavyotwezesha. Basi unapoendelea kupepeti huu moto wa Ukweli wa Injili ninaomba kwamba kamwe usiuruhusu uache kuwaka."

Ndugu Barth. C.N., Nigeria



JE, WAJUA?

Kuna makabila ya watu 17,400 ulimwenguni kote. Asilimia 42.1% ya makabila hayo haijafikiwa na Injili. Bara Hindi, Pakistani, na Uchina ndio nchi zilizo na idadi kubwa zaidi ya makabila ambayo haijafikiwa na Injili. Leo hii kuna idadi kubwa zaidi ya watu ambao hawamjui Kristo kuliko wakati mwingine wote katika historia ya ulimwengu.


Nukuu hii imetolewa kutoka kwa Mradi wa Yoshua (Joshua Project) 2022



ZIFUATAZO NI NUKUU KUTOKA KWA TOLEO ZA HAPO AWALI

“Kuna mabadiliko ya kimuujiza wakati mtu ameokoka (kwa kweli) kupitia kwa nguvu zake Yesu Kristo. Mkristo, mfuasi wa Yesu Kristo, anaweza kufuata mfano wake na kuishi bila kutenda dhambi (1 Petro 2:21-22). (Watu) wengi katika ulimwengu wa kidini wamefanya ukweli huu rahisi wa mafundisho ya Kikristo kuwa hafifu ili kutoa kisingizio cha wao kutenda dhambi.” *Toleo la 2, Dhambi na Wokovu.*

“Kujazwa kwa Roho Mtakatifu ni kazi ya imani na haiji kwa njia ya (Yeye) kujidhihirisha kwa kiwango kikubwa ama kwa hisia nyingi.”
“Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu.”
Toleo la 8, Kujazwa na Roho Mtakatifu.



“Mkristo akimsifu Bwana kwa kupaza sauti, ushuhuda, na nyimbo, yote hayo hufungua malango na kumwezesha mtu kufika kwenye uwepo wake Mungu, kwa maana Yeye hudumu katika sifa za watu wake.” *Toleo la 30, Sifa.*

“Laana ya kifo ilikuwa ya aina mbili – laana ya kiroho na ya kimwili.” “Adhabu ya kifo cha kiroho ikaondolewa kwa njia ya msamaha tupatao kutoka kwa Yesu Kristo.” *Toleo la 29, Kifo cha Kwanza na cha Pili (Pamoja) na Ufufuo.*

“Kama wasimamizi wa fedha za Mungu, fedha tulizo nazo zinahitaji kuongozwa na kushughulikiwa kwa makini na kwa uaminifu kama kwamba (hili) ni jambo la kiroho.” *Tolea la 27, Fedha.*

“Kuna tofauti kubwa kati ya majukumu ambayo mtoto wa Mungu ambaye anaishi katika neema (anahitaji kufanya) yakilinganishwa na majukumu ambayo serikali imepewa na Mungu . . . ambayo hufanywa kwa njia ya kimwili.”
Toleo la 26, Mafundisho ya Biblia Kuhusu Kutompinga Mtu Mwovu.

“Pasipo mtu kujichunguza kwa kuongozwa na mwelekeo wa kumwogopa Mungu, yeye atajipata kwamba amejihadaa mwenyewe. Haitoshi kusikia Neno; ni lazima tuwe watendaji wa Neno au tutajihadaa (sisi) wenyewe.”
Toleo la 23, Kujichunguza Kibinafsi kwa Mambo ya Kiroho.

“Sabato ya kweli ya Mkristo katika kipindi cha Agano Jipya ni jambo (liletalo) amani, pumziko, ibada za kiroho, na kuishi kwa utakatifu kila siku ya wiki. Kila siku ni takatifu na imetengwa kwa ajili ya ibada na ukumbusho wa ukombozi wa (kuacha) dhambi kupitia kwa Yesu Kristo.” *Toleo la 20, Sabato.*

“Hatuwezi kamwe kumtarajia Mungu kudhihirisha mapenzi yake katika sehemu moja ya maisha yetu (na) ambayo tunamtaka atuongoze, ilhali hatuwi watiifu kufuata kile ambacho (tayari) twajua ni mapenzi yake katika sehemu zingine za maisha yetu.” *Toleo la 40, Vile Unaweza Kujua Mapenzi ya Mungu.*

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA